

TANGAZO KWA UMMA



DEPOSIT INSURANCE BOARD

KATIKA SHAURI LA FBME BANK LIMITED (ILIYO CHINI YA UFILISI)

Taarifa inatolewa kwa umma na Deposit Insurance Board (DIB) kuwakumbusha wenye amana wa iliyokuwa **FBME BANK LIMITED** kwamba;

1. Zoezi la ulipaji wa fidia ya bima ya amana kwa mujibu wa sheria kwa wale ambao bado hawajalipwa fidia linaendelea kupitia yaliyokuwa Makao Makuu ya FBME Bank Limited yaliyopo Kinondoni, Dar es salaam.
2. Hadi mwisho wa Aprili, 2020, Deposit Insurance Board imelipa fidia kwa asilimia 51.77% ya wateja wanaostahili fidia na asilimia iliyobakia bado hawajajitokeza kuchukua fidia hiyo.
3. Kwa tangazo hili, Deposit Insurance Board inarudia kuwakumbusha wateja wote ambao hawajachukua fidia ya bima ya amana, kufika kwenye yaliyokuwa Makao Makuu ya FBME Bank Limited yaliyopo Kinondoni, Dar es salaam ili kulipwa fidia zao.

UKISIKIA TANGAZO HILI TAFADHALI MTAARIFU NA MWENZIO.

TANGAZO HILI LIMETOLEWA TAREHE 22 MEI 2020

**MKURUGENZI
DEPOSIT INSURANCE BOARD
JENGO LA MAKAO MAKUU YA BENKI KUU YA TANZANIA
2 MTA A WA MIRAMBO
GHOROF A YA 11, MNARA WA KASKAZINI
11884 DAR ES SALAAM**

**BARUA PEPE: DIB-INFO@BOT.GO.TZ
SIMU YA MEZANI: +255 22 223 5390
Fax: +255 22 223 4200**